BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Pili – Tarehe 30 Novemba, 2023.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017 na Kutunga Sheria ya Mahakama za Kadhi na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017 na Kutunga Sheria ya Mahakama za Kadhi na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

51. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

    Je, tathmini ya idadi ya watumiaji wa madawa ya kulevya katika ngazi za vijiji vyetu iko vipi.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

87. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

    Moja ya malengo ya Serikali ni kuwatambua na kuwaenzi wazee ambao wamefikia umri wa miaka 70 kwa kuwapatia fedha kwa ajili ya kuwapunguzia ukali wa maisha kwa kila mwezi. Lakini fedha hizi zimekuwa na usumbufu mkubwa sana kwa wazee hao hasa wanaotoka vijiji vya shamba ambako huduma za benki hazipatikani.

    (a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kujenga Tawi la benki ya PBZ katika maeneo ya Nungwi, ili kuwasaidia Wazee kupokea fedha zao kwa urahisi.

    (b) Kwa kuwa kuna baadhi ya wazee wamekimbia na kuzisamehe fedha za malipo ya mwezi wa Oktoba, 2023. Je, Wizara yako inatoa kauli gani kwa wazee hao.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

28. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

    Tathmini iko vipi juu ya kupatikana ajira rasmi na zisizo rasmi kwa watu wenye mahitaji maalum.

**Wizara ya Afya:**

31. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Idadi ya ongezeko la matatizo ya afya ya akili hailingani na idadi ya wataalamu au wanasaikolojia wa kutosheleza wa kukidhi utatuzi wa tatizo hili.

Je, ni upi Mpango Mkakati wa Wizara yako wa kuwa na wanasaikolojia wa kutosha watakaoweza kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wa afya ya akili nchini kwetu.

83. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya kilichopo Masingini ni kituo kimoja wapo miongoni mwa vituo vinavyotoa mchango mkubwa sana katika kuwapatia huduma za afya wananchi wanaoishi karibu na kituo hicho, ingawa kituo hicho hakipo katika hali nzuri.

(a) Ni lini kituo hiki kitafanyiwa matengenezo makubwa ili kiweze kutoa huduma zilizo bora zaidi.

(b) Ni motisha ya aina gani wanayopatiwa madaktari waliopo kituoni hapo katika kuhakikisha kwamba wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

85. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake): Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na kufanya vizuri kwa Wizara yako katika kutoa huduma kwa wananchi, Kitengo cha Uzazi cha Hospitali ya Mnazi Mmoja bado kiko nyuma katika kuwapatia huduma zilizo bora wananchi wanaofika kuhudumiwa kituoni hapo.

Je, ni madaktari wangapi hadi sasa tayari wameshachukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria ambao wamekumbwa na makosa ya kuwanyanyasa na kuwapuuza wagonjwa wanaofika kupata huduma kituoni hapo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

11. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kwa kuwa kumekuwa na uhaba mkubwa wa walimu wa sayansi na kwa kuwa Chuo cha Kiislamu ndio chuo pekee kwa Unguja na Pemba kinachotoa uwalimu. Na kwa kuwa wanaojiunga na Chuo cha Kiislamu wanatakiwa wawe na ufaulu wa chini wa Form IV na ndio maana kukawa na mrundikano wa walimu wa 'Art' na uhaba mkubwa wa walimu wa sayansi.

    (a) Je, Wizara yako ina mkakati upi wa kuwasomesha vijana wetu kozi za ualimu wa sayansi.

    (b) Je, ni lini Serikali itaanzisha chuo chengine cha ualimu na kuchukuwa wanafunzi wenye Divisheni I, II, au III kwa lengo la kupata walimu bora wenye ufanisi na kupunguza uhaba wa walimu wa sayansi nchini.

    (c) Je, ni upi mkakati endelevu wa Wizara kuzalisha walimu wa sayansi.

40. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kwa tathmini ni masomo gani wanafunzi wetu hususan wa kidato cha nne na cha sita wamekuwa hawafaulu vizuri na ni kwa sababu gani za msingi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

62. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    Je, kuna hatua gani mpaka sasa zinazoendelea katika ukarabati wa jengo maarufu la kihistoria la Beit al-Ajaib.

63. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    (a) Ni lini Makumbusho ya "Peace Memorial" yaliyopo eneo la Mnazi Mmoja yatazinduliwa rasmi na kuanza kutumika.

    (b) Je, ni changamoto gani zinazopelekea ucheleweshaji wa uzinduzi huo.

**III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>**

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017 na Kutunga Sheria ya Mahakama za Kadhi na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**30 Novemba, 2023.**

**Raya Issa Msellem**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**